AJALI

"Ni kweli kuna ajali imetokea katika Wilaya ya Bahi ikihusisha mabasi mawili ya abiria, chanzo na nini limetokea, nitawajulishe kupitia taarifa kwa umma, naomba uvute subira."

Kamanda Gallus Hyera



Ajali iliyohusisha mabasi mawili yaliyogongana katika eneo la Ibihwa Wilaya ya Bahi, mkoani Dodoma na kusababisha vifo na majeruhiwa, jana. **Na Mpigapicha Maalumu**

# Ajali zilivyokatiza uhai wa watu 14 ndani ya siku nne

Waandishi Wetu, Mwananchi
mwananchipapers@mwananchi.co.tz

Dar/mikoani. Matukio mawili ya ajali yaliyoripotiwa kutokea ndani ya siku nne yamepoteza uhai wa watu 14, huku ikiwajeruhi wengine 71 katika maeneo mbalimbali nchini.

Idadi hiyo ya vifo vya ajali ni sawa na wastani wa karibu watu wanne kila siku.

Hata hivyo, idadi hiyo haihusishi matukio ambayo hayajaripotiwa.

Ajali hizo, zimetokea kati ya Julai 30 na Agosti 2, mwaka huu, huku zote zikitokana na magari kugongana, katika Wilaya ya Bahi mkoani Dodoma na nyingine Monduli, Arusha.

Matukio hayo ndio yaliyopoteza uhai wa wengi zaidi kwa wakati mmoja, ukilinganisha na ajali nyingine mbalimbali zilizotokea ndani ya mwaka huu.

**Ajali iliyoua wanane**

Katika Wilaya ya Bahi mkoani Dodoma jana, watu wanane walifariki dunia na wengine 66 kujeruhiwa kutokana na ajali iliyohusisha mabasi mawili yaliyogongana.

Ajali hiyo ilihusisha basi la Kampuni ya Isamilo, lililokuwa likitokea Mwanza kuelekea Dar es Salaam na Basi la Libanika Luxury, lililokuwa likitoka Dar es Salaam kuelekea Mwanza.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Gallus Hyera alithibitisha kutokea kwa ajali hiyo.

"Ni kweli kuna ajali imetokea katika Wilaya ya Bahi ikihusisha mabasi mawili ya abiria, chanzo na nini limetokea, nitawajulishe kupitia taarifa kwa umma, naomba uvute subira," alisema alipozungumza na Mwananchi.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule alithibitisha vifo vya watu wanane, akisema kati yao wanaume ni watano na wanawake watatu.

"Kwa masikitiko tumepoteza wenzetu katika ajali hiyo, watu saba walifariki papo hapo lakini mmoja amepoteza maisha wakati akiendelea kupatiwa matibabu katika hospitali ya rufaa ya mkoa," alisema Senyamule.

Alisema mabasi hayo yaligongana alfajiri katika Kijiji cha Ibihwa Wilaya ya Bahi, baada ya mmoja wa madereva alipokuwa akijaribu kulipita gari lililokuwa mbele yake bila kuchukua tafadhari.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma, Dk Ernest Ibenzi alikiri kuwapokea majeruhi 66 na kwamba wanaendelea na huduma katika hatua tofauti tofauti.

"Tumewapokea majeruhi 66, wengine wanatibiwa kwenye wodi za kawaida za majeruhi lakini baadhi wamepelekwa katika vyumba vya upasuaji na bado wanaendelea na kupatiwa huduma," alisema Dk Ibenzi.

**Ajali iliyoua sita**

Katika hatua nyingine, Julai 30, mwaka huu, watu sita walipoteza maisha kutokana na ajali iliyohusisha basi lililogongana na lori wilayani Monduli mkoani Arusha.

Ajali hiyo ilitokea Julai 30, saa 12:40 jioni katika barabara ya Arusha-Dodoma, Makuyuni wilayani Monduli, Mkoa wa Arusha.

Mbali na idadi hiyo ya waliopoteza maisha katika ajali hiyo, watu watano walijeruhiwa na kati yao wawili wameruhusiwa, huku watatu wakiendelea na matibabu.

Akizungumzia hilo jana, Kaimu Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Mount Meru, Dk Kipapi Mlambo alisema hadi Ijumaa mchana kulikuwa na majeruhi watatu wanaoendelea na matibabu.

Alisema wawili waliokuwa na majeraha yasiyo makubwa waliruhusiwa baada ya madaktari kuridhika na hali zao.

Alieleza majeruhi hao wanaoendelea na matibabu, mmoja amevunjika mfupa wa shingo na baada ya kufanyiwa tathmini za kitabibu ameridhia kufanyiwa upasuaji.

"Kwa huyu mfupa wa shingo umevunjika,kuna njia mbili za matibabu, kufunga ili upone wenyewe au kufanya upasuaji. Ameomba kufanyiwa upasuaji na taratibu zimekamilika, atafanyiwa kesho," alisema Dk Mlambo.

Alisema majeruhi mwingine alikuwa na majeraha ya kichwa pamoja na tatizo katika jicho, lakini anaendelea vizuri na ndugu zake tayari wamepatikana.

"Tumemshauri akae hapa kwa sababu jicho lake halijakaa vizuri kidogo,tunataka kuona maendeleo yake kabla ya kuamua hatua nyingine," alisema.

Alisema majeruhi mmoja alipata majeraha zaidi katika taya na ulimi na amepewa rufaa kwenda Hospitali ya KCMC kutokana na kuhitaji huduma ya daktari bingwa wa taya.

Alieleza kuwa, hali ya majeruhi huyo haikuruhusu kusafirishwa kwa sababu alikuwa akipata changamoto ya kupumua, lakini baada ya kuimarika ameandaliwa kupelekwa KCMC.

"Huyu wa tatu ndiye aliumia zaidi kuliko wengine, tunampa rufaa aende KCMC kwani kwa ubingwa tulionao hapa hautoshelezi kumtibu,ameshakaa vizuri leo na anaandaliwa leo apelekwe KCMC," alisema.

Ajali hiyo ilitokea usiku wa Julai 30, 2026 baada ya basi la Kampuni ya Kandahari, kugongana uso kwa uso na lori.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Justine Masejo, alisema watu sita walifariki dunia kutokana na ajali hiyo kati ya hao, watano walifariki papo hapo na mmoja alifariki wakati akipatiwa matibabu hospitalini.

Alisema waliofariki ni wanaume watatu na wanawake watatu.

Ajali hiyo, alisema ilihusisha basi hilo lililokuwa likitoka mkoani Kilimanjaro kuelekea Mpanda mkoani Katavi na lori lililokuwa likitoka Kahama mkoani Shinyanga kuelekea Tanga.

Alisema polisi wanaendelea na uchunguzi kubaini chanzo cha ajali hiyo, huku miili ya marehemu ikiwa imehifadhiwa katika Kituo cha Afya Makuyuni kwa ajili ya uchunguzi wa kitabibu na taratibu za utambuzi.

Katika tukio hilo, lori jingine lililokuwa nyuma ya lori lililogongana na basi lilipinduka baada ya dereva wake kujaribu kukwepa ajali hiyo.

Masejo, alitoa onyo kwa madereva wanaokiuka sheria za usalama barabarani, akisema vitendo kama kupita magari bila tahadhari katika maeneo yaliyokatazwa vinaweza kusababisha madhara makubwa.

"Jeshi la Polisi Mkoa wa Arusha linatoa onyo kwa baadhi ya madereva wasiozingatia sheria za usalama barabarani, ikiwamo kupita magari mengine bila tahadhari au sehemu ambazo alama na michoro ya barabara imekataza kufanya hivyo," alisema.

Baada ya ajali hiyo, Jeshi la Polisi, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji pamoja na wananchi walifika eneo la tukio kusaidia kuwaokoa majeruhi waliokuwa wamenasa ndani ya magari na kutoa miili ya marehemu kwa ajili ya kutambuliwa na ndugu zao.

**Imeandikwa na Janeth Mushi, Habel Chidawali na Filbert Rweyemamu**

**USULI**

**Ndani ya siku nne, ajali mbili za barabarani zilizotokea mikoa ya Dodoma na Arusha na kusababisha vifo vya watu 14 na kujeruhi wengine 71. Tukio la Bahi limeua watu wanane na kujeruhi 66, huku ajali ya Monduli ikisababisha vifo vya sita na majeruhi watano. Matukio hayo yamekuwa miongoni mwa ajali zenye madhara zaidi kuripotiwa mwaka huu, huku mamlaka zikisisitiza umuhimu wa madereva kuzingatia sheria za usalama barabarani ili kuepusha vifo na majeraha yanayotokana na ajali.**

UHURU Jumatatu Agosti 3, 2026

# Mabasi yagongana, wanane wafariki dunia

**Na FRED ALFRED,** *Dodoma*

WATU wanane wamefariki dunia na wengine 66 kujeruhiwa, baada ya mabasi mawili kugongana uso kwa uso katika eneo la Ibihwa, Halmashauri ya Wilaya ya Bahi, mkoani Dodoma.

Akizungumza jijini hapa jana, Kaimu Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Rehema Jeremia, amethibitisha kutokea ajali hiyo.

Alisema ajali hiyo ilihusisha basi la Isamilo, lenye namba za usajili T 428 EXP, lililokuwa likitokea Mwanza kwenda Dar es Salaam, na basi la Libanika Luxury, lenye namba za usajili T 897 DUP, lililokuwa likitokea Dar es Salaam kwenda Mwanza.

Akizungumza baada ya kuwatembelea majeruhi katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma, Mkuu wa Mkoa huo, Rosemary Senyamule, alisema watu saba walifariki dunia papo hapo katika eneo la tukio na mmoja baadaye alipokuwa akipatiwa matibabu hospitalini.

Senyamule alisema kati ya majeruhi 66, watu tisa wana hali mbaya na majeruhi 57 hali zao zikiendelea vizuri.

Alisema majeruhi hao wapo katika hospitali tatu tofauti ambazo ni Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma, Hospitali ya Makole na Hospitali ya Wilaya ya Bahi, kwa ajili ya kupatiwa matibabu.

Kwa mujibu wa Mkuu huyo wa Mkoa, uchunguzi wa awali unaonesha chanzo cha ajali hiyo ni dereva mmoja kujaribu kuipita gari jingine bila kuchukua tahadhari hatua iliyosababisha mabasi hayo kugongana uso kwa uso.

Mmoja wa majeruhi, Jail Martin, alisema ajali hiyo ilitokea saa 12 asubuhi.

Alisema waliona basi walilokuwa wakisafiria likianza kuyumba kabla ya kugongana uso kwa uso na basi lililokuwa likitokea upande wa pili.

# Watu 9 wafa ajali ya mabasi Dodoma

Na Rehema Lugono

WATU tisa wamekufa na wengine 66 wamejeruhiwa baada ya mabasi mawili kugongana uso kwa uso eneo la Ibihwa, Wilaya ya Bahi mkoani Dodoma.

Mabasi hayo likiwemo la Kampuni ya Isamilo namba T428 EPX lililokuwa likitoka Mwanza kwenda Dar es Salaam na basi la Libanika Luxury namba T897 DUP lililokuwa likitoka Dar es Salaam kwenda Mwanza, yaligongana jana saa 12.00 asubuhi.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule alisema katika ajali hiyo walikufa wanaume watano na wanawake wanne na kueleza kuwa majeruhi tisa walikuwa na hali mbaya na majeruhi waliendelea kutibiwa katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma na Hospitali ya Wilaya ya Bahi.

Alihimiza madereva wazingatie sheria za usalama barabarani ikiwa ni pamoja na kuendesha kwa tahadhari.

Kaimu Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Rehema Menda alisema vyombo vya ulinzi na usalama vinaendelea na uchunguzi kubaini chanzo cha ajali.

Majeruhi wakiwa Hospitali ya Rufaa ya Dodoma walidai chanzo cha ajali hiyo ni mwendo kasi wa moja ya mabasi hayo.

Majeruhi mkazi wa Singida, Jaeli Martine alidai dereva wa basi alilopanda alijaribu kulipita lori lililokuwa mbele yake lakini katika jitihada za kulikwepa alijikuta akigongana uso kwa uso na basi lililokuwa likitoka upande wa pili wa barabara.

Abiria mwingine mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Zabroni Kamaniga alidai walipotika katika Kijiji cha Bahi aliona basi likihama njia na kugongana uso kwa uso na basi alilokuwa amepanda.